

Athari za Ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora

- Matumizi mabaya ya rasilimali za nchi
- Kuongezeka kwa umasikini, ujinga na maradhi
- Kuongezeka kwa rushwa
- Huduma mbovu za jamii
- Kuhatarisha amani na utulivu
- Kutoheshimiwa kwa haki za binadamu
- Kuongezeka kwa dhuluma na uonevu.

Changamoto za Utawala Bora

Changamoto za utawala bora ni nyingi katika uendeshaji wa sekta za umma hapa nchini. Baadhi yake ni kama zifuatazo:

Rushwa

Pamoja na hatua na mikakati mbalimbali kuundwa ili kukabili suala la rushwa tatizo hili linapungua kwa kiwango kidogo sana. Hivyo mikakati madhubuti zaidi inahitajika kukabiliana na tatizo hili ili kulifuta kabisa katika jamii.

Kukosekana kwa ushiriki na ushirikishwaji

Viongozi kutoshirikisha jamii na wadau mbalimbali katika miradi na shughuli za maendeleo kunasababisha utawala bora kutotekelzeza kwa urahisi katika ngazi mbalimbali.

Ukosefu wa uwajibikaji na uwazi

Mfano: Kwenye mikataba mbalimbali, uwajibikaji mdogo kwenye sekta za umma.

Ukosefu wa wataalamu wa fani mbalimbali katika maeneo mengi, hususan ya vijijini. Mfano: wataalamu wa kilimo, afya, elimu, miundombinu n.k.

Kutoheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Kimetolewa na:

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
Kitalu Na. 339 Mtaa wa Nyerere/Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978
Barua Pepe: info@chrarrg.go.tz;
Tovuti: www.chrarrg.go.tz

UTAWALA BORA

(Dhana, misingi na umuhimu)

Maana ya Dhana Muhimu

Mtawala

Ni mtu aliyeaminiwa na kupewa dhamana ya matumizi ya mamlaka kisiasa, kiuchumi au vinginevyo katika kusimamia rasilimali za umma. Pia ni mtu aliyepewa dhamana ya kufanya maamuzi ya kimamlaka kwa faida ya jamii.

Utawala

Utawala (Governance) unaweza kuelezwu kuwa; ni matumizi ya mamlaka kisiasa, kiuchumi au vinginevyo katika kusimamia rasilimali za Taifa. Vilevile utawala ni mpango wa kufanya maamuzi ya kimamlaka kwa faida ya jamii yenye mwelekeo, udhibiti na usimamizi wa rasilimali za umma.

Utawala Bora

Utawala bora ni “zoezi la wenyewe madaraka katika maamuzi kuamua ni namna gani rasilimali za taifa zitumike kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi”. Mfumo huo unaendelea kueleza kwamba utawala bora unataka jamii iendeshe mambo yake kwa kuzingatia misingi ya uwazi, matakwa ya wengi, uwajibikaji na pale ambapo watendaji katika utumishi wa umma wana uwezo wa kufanyakazi kwa ufanisi na uadilifu na wanatumia ujuzi wao kwa manufaa ya jamii.

“Na waachiwe watawala wale tu wenyewe uwezo wa kutawala vyema. Tunapambana ili tuishi kwa amani...” - Aristotle -

Viongozi lazima wazingatie mambo yafuatayo:

- **Matumizi sahihi ya dola**
- **Matumizi mazuri ya madaraka yao**
- **Kujua na kutambua madaraka waliyonayo na matumizi yake**
- **Madaraka yanatumika kulingana na mipaka iliyowekwa na katiba na sheria.**

Misingi ya Utawala Bora

Misingi ya utawala bora imejengwa na:

- Ushirikishwaji (Participation)
- Maridhiano (Consensus Orientation)
- Mwitikio (Responsiveness)
- Matokeo bora na ufanisi (Effectiveness and Efficiency)
- Uwajibikaji (Accountability)
- Uwazi (Transparency)
- Usawa (Equity)
- Utawala wa Sheria (Rule of Law)
- Maono ya Kimkakati (Strategic Vision)
- Uadilifu (Integrity).

Nguzo za Utawala Bora

Dhana ya utawala bora ni dhana ambayo inatokana na nguzo mbalimbali za utawala ambazo zimekuwepo duniani tangu kuanza kwa ustaarabu. Kuna nguzo kuu sita, nazo ni:

- Katiba ya kidemokrasia yenye ridhaa ya wananchi (Democratic Constitution)
- Kulinda, kukuza na kuheshimu haki za binadamu (Protection, promotion and respect for human rights)
- Utawala wa Sheria (Rule of Law)
- Mgawanyo wa Madaraka (Separation of powers)
- Uhuru wa Mahakama (Independence of the judiciary)
- Uhuru wa habari na uhuru wa vyombo vya habari (Freedom of expression and the freedom of the press).

Umuhimu wa Utawala Bora

Katika ngazi yoyote ile ya uongozi kuanzia Kitongoji, Kijiji, Halmashauri, hadi ngazi za kitaifa, utawala bora ni muhimu; kwani unasaidia kuwa na mambo yafuatayo:

- Matumizi mazuri ya rasilimali za nchi
- Maendeleo endelevu
- Kupungua kwa umasikini, ujinga na maradhi
- Kutokomea kwa rushwa
- Huduma bora za jamii
- Amani na utulivu
- Kuheshimiwa kwa haki za binadamu
- Utatuizi wa migogoro kwa mujibu wa sheria na taratibu.